

Seattle Cancer Care Alliance

Gari la Mammogramu

Njia inayofikika kwa urahisi ya kupata uchunguzi unaohitaji.



Ili kuratibu uchunguzi wako piga simu kwa
(206) 606-7800

Kwa maelezo zaidi, ikiwa ni pamoja na
maeneo ambayo gari linapatikana, tembelea
www.SeattleCCA.org/mammography

Je, ulijua?

- Miadi huchukua dakika 15 tu.
- Huhitaji rufaa kwa mammogramu ya uchunguzi wa kila mwaka.

Ustahiki

- Unastahiki kupata mammogramu ikiwa wewe ni mwanamke na:
- Una umri wa miaka 40 na zaidi
- Hujafanya mammogramu kwa mwaka mmoja uliopita
- Huna dalili zozote katika matiti yako

Tafadhali leta:

- Kadi yako ya bima ya afya. Mipango mingi ya bima hutoa mammogramu ya kila mwaka lakini tafadhali wasiliana na mtoaji wa bima yako ya afya **kabla ya miadi yako** ili kuthibitisha ustahiki wako.
- Kitambulisho cha picha
- Jina, nambari ya simu na anwani ya mtoa huduma wako wa msingi wa matibabu.



Je, unahitaji mkalimani?

Kwa Kihispania, Kimandari, Kivietinamu, Kirusi na Kikorea, piga simu kwa 1 (855) 670-9798. Kwa lugha nyingine zote, piga simu kwa (206) 606-7800. Sema jina la lugha yako. Subiri hadi mkalimani ajiunge katika simu yako.



Mpango wa Seattle Cancer Care Alliance Breast Imaging ni Kituo Bora cha Upigaji Picha wa Matiti kilichoidhinishwa kinachotoa teknolojia bora ya kisasa ya kidijitali na wataalamu wa radiolojia waliojitolea kwa dhati kwa afya ya matiti pekee.

**Seattle
Cancer Care
Alliance**

Fred Hutch · Seattle Children's · UW Medicine